

# Jinsi ya kutayarisha Mbolea Vunde/ Mboji

Mti hutoa hifadhi na kivuli

Huwa tayari banda ya  
 waiki  
**6+**  
 na zaidi

Mbolea vunde hutengenezwa kwa kuchanganya matabaka tofauti tofauti ya masalia ya mazao. Kadri masalia yanavyooseshwa ndivyo huwa mbolea vunde. Kuna njia nyingi tofauti za kutengeneza mbolea vunde. Hii ni njia moja wapo.



**1** Majani makavu huupa udongo kaboni na kuboresha mfumo/ mpangilio wa udongo

**2** Nyunyizia maji kusaidia biwi kuoza

**3** Samadi kutoka kwa wanyama mfano Ng'ombe, kuku, mbuzi, au sungura huongeza rutuba

Kufunika hukinga na kufanya mbolea vunde iwe na unyevunyevu

Tumia pima joto kuangalia kuwa biwi linaoza

Nyunyizia jivu kwa ajili ya madini ya potashiamu na maji ili kusaidia biwi kuoza

**5** Mimea ya kijani/ mibichi huongeza virutubisho

**4** Udongo wa juu wenye rutuba kwa wadudu na chambo (minyoo wa kwenye udongo)

Chimba shimo na tayarisha msingi kwa kutumia vitawi au mabua



**Tayarisha msingi**

- Tafuta sehemu yenye kivuli
- Chimba shimo kwaajili ya mbolea vunde
- Tayarisha msingi kwa kutumia vitawi au mabua



**Panga matabaka**

- Katakata majani na panga matabaka
- Rudia kila tabaka mara 3 au 4
- Funika kwa udongo na nyasi kavu



**Geuza biwi**

- Baada ya wiki 3 geuza biwi tabaka kwa tabaka
- Hii husaidia mbolea vunde kuiva
- Geuza tena baada ya wiki 3
- Baada ya wiki nyingine 3. itakuwa tayari



**Matumizi kweye mimea**

- Huwa tayari kama Biwi likiwa hudhurungi na tufufu
- Chimba shimo kuzunguka mimea, weka mbolea vunde kisha funika

**Kwa nini Kutumia mbolea vunde?**

- inaongeza mavuno
- ni mbolea ya bure ya kilimo hai
- inawezesha kurudia kimatumizi mabaki ya viumbe hai
- inawasaidia viumbe hai kwenye udongo
- inaboresha muundo wa udongo
- inahifadhi virutubisho kwa muda mrefu
- ina uwezo mkubwa wa kutunza maji
- inaua wadudu na magonjwa katika udongo

**Ongeza mavuno yako kwa kutumia mboji!**

